TANGAZO LA SERIKALI NA. 29 la tarehe 20/1/2023

SHERIA YA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE

(SURA 373)

# NOTISI

(*Imetengezwa chini ya kifungu cha 3(1))*

NOTISI YA TANGAZO LA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE, 2023

Sura ya 373

KWA KUWA, kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kanda za Uzalisha kwa Mauzo ya Nje, kinampa mamlaka Waziri, kwa ushauri wa Bodi na kwa kushaurina na Mamlaka husika na kwa mapendekezo ya Mamlaka (EPZA), kwa Notisi iitakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali-;

(a) kuanzisha au kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa eneo la Kanda ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje; na

(b) kuamua eneo, ukubwa na sifa halisi za mipaka ya eneo la Kanda ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje

NA KWA KUWA, Bodi ya Mamlaka ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje imemshauri Waziri kutangaza maeneo ya ardhi kuwa Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje;

NA KWA KUWA Waziri baada ya kushauriwa, alishauriana na Mamlaka husika na Mamlaka hizo kuridhia kutangazwa kuwa Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje kwa maeneo yafuatayo Eneo la Dundani, Wilaya ya Mkuranga, Mkowa wa Pwani, Vijiji vya Mavuji, Nainokwe, Liwiti na Migeregere, Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi, Eneo la Viwanda Zegereni Wilaya ya Kibaha, Mkowa wa Pwani, na Eneo la Mmovo, Kata ya Kitangari,Wilaya ya Newala, Mkowa wa Mtwara;

Sura ya 373

HIVYO BASI, katika utekelezaji wa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kanda za Uzalisha kwa Mauzo ya Nje, Mimi, ASHATU K. KIJAJI, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, natangaza maeneo yaliyotajwa kwenye Notisi hii kuwa Kanda za Uzalisha kwa Mauzo ya Nje kama ifuatavyo-

Jina

1. Tangazo hili litajulikana kama Notisi ya Tamko la Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje , ya mwaka 2023 na itaanza kutumika katika tarehe itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Tamko la Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje

2. Maeneo ya ardhi yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hili yanatangazwa kuwa Maeneo ya Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MAENEO YALIYOTANGAZWA KUWA KANDA ZA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eneo: | Eneo la Dundani lililopo Wilaya ya Mkuranga, Mkowa wa Pwani. |
| | Kiwanja Na: | 16 - 19, Kitalu. |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 24,352 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Mamlaka ya EPZ |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Tan-Ko Mirae Green |
| 2. | Eneo: | Vijiji vya Mavuji, Nainokwe, Liwiti na Migeregere vilivyopo Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi |
| | Shamba Na: | 814, 815, 824, 825, na 826. |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 4054 Ha, 4788.452Ha, 6,000 Ha. na 10,000Ha. |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Mamlaka ya EPZ |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Pan Tanzania |
| 3. | Eneo: | Eneo la Viwanda Zegereni lililopo Wilaya ya Kibaha, Mkowa wa Pwani. |
| | Kiwanja Na: | 9, Kitalu "A" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | Ekari 2.6. |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Mamlaka ya EPZ |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Gravita Tanzania |
| 4. | Eneo: | Eneo la Mmovo, Kata ya Kitangari iliyopo Wilaya ya Newala, Mkowa wa Mtwara |
| | Kiwanja Na: | 1, Kitalu "B" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 99,883 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | TENACU Intergraded Resources Limited. |
| | Jina la aliyepewa: | Ukanda wa Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Tanecu Holdings |

Dodoma,
30 Desemba, 2022.

ASHATU K. KIJAJI,
*Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara*